

HALMASHAURI YA WILAYA TUNDURU

SHULE YA SEKONDARI MTUTURA
S. L.P. 84
MOB: 0685873232
TUNDURU

KUMB. NA. MT/SS/2019

20/12/2019

JINA LA MWANAFUNZI:

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MTUTURA WILAYA YA TUNDURU MKOA WA RUVUMA MWAKA 2020

1.0.UTANGULIZI

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidate cha kwanza katika shule ya sekondari Mtutura. Shule hii ipo katika kata ya namiungo karibu na shirika la Wamisionari la Mungu Mwokozi. Unatakiwa kuripoti shuleni siku ya Jumatatu tarehe **06/01/2019** saa **1:30 asubuhi** ukiwa na mzazi /mlezi wako.

2.0.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. Sare za shule

(a) (i) Wavulana

Suruali ya rangi ya damu ya mzee mbili (2) na mashati meupe mikono mifupi mawili (2). Suruali na mashati mtindo wa **MODO haziruhusiwi hapa shuleni**. Viatu rangi nyeusi vya ngozi jozi mbili na soksi nyeusi jozi mbili.

(ii) Wasichana

Sketi rangi ya damu ya mzee mbili (2) mshono wa rinda na mashati meupe mikono mifupi mawili (2). Viatu vya ngozi rangi nyeusi jozi mbili na soksi nyeupe jozi mbili. Vazi la **HIJABU** kwa wasichana wanaopenda kuvaa lishonwe kwa kitambaa cha sare ya shule kama ifuatavyo:-

Sketi ndefu mbili (2), nusu kanzu mbili (2) mikono mirefu na kitambaa cheupe cha kufunga kichwani.

NB: Viatu vyenye visigino virefu au mchuchumio havitakiwi.

(b) Sare ya michezo kwa shule hii ni kama ifuatavyo:-

- Wavulana

Bukta rangi ya bluu moja (1), fulana ya bluu moja (1), viatu vya raba za michezo jozi moja (1) na soksi ndefu (stocking) jozi mbili (2)

- Wasichana

Suruali ya traksuti nyeusi moja (1), fulana ya bluu moja (1), viatu vya raba za michezo jozi moja (1) na soksi ndefu (stocking) jozi mbili (2).

(c) Nguo za kuvaa nje ya darasa (za kazi)

Suruali nyeusi kwa wavulana na sketi nyeusi mshono wa rinda kwa wasichana na fulana ya bluu (wote)

2.2.Madaftari makubwa yasiyopungua 15, kalamu (peni), penseli na mkebe wa hesabu (Mathematical set)

2.3.Utaratibu wa chakula utaelekezwa baadae.

2.4.Mahitaji mengine ya Kibinadamu: Aje na vifaa vya usafi kama

NB: Suala la Matibabu kwa mwanafunzi ni jukumu la mzazi. Unatakiwa kuacha namba ya simu shuleni ili moto akiugua upate taarifa.

3.0. Sheria na kanuni za shule.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- d) Kuwahi katika kila shughuli na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;-
- i) Kutunza mali za Umma.

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule.

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile:- uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- d) Kupigana au kupiga
- e) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- f) Kudharau Bendera ya Taifa
- g) Kuwa mjamzito/kupata mimba
- h) Kuoia au kuolewa
- i) Kutoa mimba
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- l) Kuwa na simu ya mkononi
- m) Kukata miti eneo la shule bila ruhusa au kibali

NB: Hakikisha unapima afya yako katika Hospitali ya Serikali. Fomu imeambatanishwa kisha rudisha shuleni.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

.....
MKUU WA SHULE

MTUTURA

**HEADMASTER
MTUTURA SEC SCHOOL
P.O. BOX -
TUNDURU**